Jamhuri ya Muungano wa Tamnzania

DodomaYetu Wiki Hii

Toleo Na: 001 - **Juni 13 -19, 2022**

Jarida maridhawa la mtandaoni la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

Yaliyojiri wiki hii Katika Makao Makuu ya Nchi

Mhe. Mtaka aongea na madereva bodaboda na bajaji

Mkuu wa mkoa wa Dodoma, Mhe. Anthony Mtaka alikutana na madereva wa pikipiki maarufu kama bodaboda pamoja na wale wanaoendesha bajaji mwezi Mei, 2022, katika ukumbi wa Cavillum uliopo Jijini Dodoma. Lengo likiwa ni kuongea na kupanga mikakati ya kuimarisha ulinzi na usalama wa mkoa kutokana na kukithiri kwa matukio ya unyang'anyi yanayohusisha madereva wa vyombo hivyo.

Katika kikao hicho madereva hao walipata fursa ya kuwasilisha kero mbalimbali wanazokumbana nazo katika suala zima la usalama barabarani wakiwa katika shughuli za kujitafutia riziki ikiwemo malipo ya faini zisizo na risiti, kubambikiwa kesi na kero nyingine kadhaa.

Mamlaka husika kama TARURA, LATRA na askari wa usalama barabarani, walipata nafasi ya kujibu baadhi ya kero na kuzitolea ufafanuzi na mwisho Mhe. Mtaka alikamilisha kwa kuvitaka vyombo husika kuheshimu watu wanaojitafutia rikizi zao kihalali kwa kutoa wito wa kusitishwa mara moja kwa sheria kandamizi na kusisitiza kuwa Mkoa unatengeneza kundi jipya la wafanyabiashara wa kimtandao miongoni mwao ni madereva wa bodaboda na bajaji.

Mkuu wa Mkoa Dodoma - Mhe. Anthony Mtaka (picha ndogo juu), akiongea na viongozi pamoja na madereva wa bajaji na Bodaboda jijini Dodoma.

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma yatoa msaada kwa Mariam Mchiwa

Mariam Mchiwa, binti mwenye umri wa miaka 19, Mwenyeji wa Kijiji cha Songambele Mkoa wa Dodoma ambaye alihitimu elimu ya Kidato cha Nne mwaka 2021 kwa kupata ufaulu wa daraja la kwanza amefika kwenye ofisi ya Mkoa wa Dodoma kuitika wito wa Mkuu wa mkoa wa Dodoma Mhe. Anthony Mtaka baada ya taarifa za uhitaji wa msaada wa kuendelezwa kimasomo kidato cha Tano na Sita kumfikia.

Mariam ambaye anatoka kwenye familia yenye hali ngumu kiuchumi, baada ya kuhitimu Kidato cha Nne, aliamua kujishughulisha na vibarua vidogo vidogo na baada ya matokeo ya Kidato cha Nne kutoka na kufanikiwa kupata ufaulu mzuri, alisafiri kwenda jijini Dar es Salaam kufanya shughuli za ndani kwa Bi Agnes Kosamu akiwa na lengo la kukusanya fedha ili aweze kurudi kujiendeleza na masomo ya Kidato cha Tano kwa kuwa familia yake haina uwezo wa kumuendeleza.

Mhe. Mtaka aliwashukuru wadau mbalimbali waliojitokeza kumsaidia Mariam ikiwa ni pamoja na Spika mstaafu na Mbunge wa Kongwa Mhe. Job Ndugai ambaye kwa sasa binti huyo anaishi nyumbani kwake, aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Maabara ya Taifa Bw. Nyambura Moremi, Chuo Kikuu cha Mwanza, Equity Bank pamoja na wengine watakaoendelea kujitokeza kumsaidia Mariam ambaye malengo yake ni kuja kuwa Muuguzi.

Mhe. Mtaka alisema kuwa Ofisi yake itahakikisha inampatia Mariam mahitaji yake yote yatakayomuwezesha kumaliza Kidato cha Sita. Aidha amewataka wanafunzi wote wanaokabiliwa na changamoto mbalimbali hususani wale ambao wamemaliza Kidato cha Nne katika shule za kata na kuchaguliwa kujiunga Kidato cha Tano, wawasiliane na Ofisi za Wakuu wa Wilaya katika maeneo waliyopo na kisha kuwasiliana na Afisa Elimu wa maeneo hayo ili kuelezea changamoto zao na kuona namna bora ya kuwasaidia.

Mhe. Mtaka ametoa angalizo kwa wazazi kutokutumia wito huo vibaya na kukwepa majukumu yao kwa kujifanya wajane na wagane wa muda na hata yatima wa muda. Pia amemtaka mwanafunzi Mariam kuwa na moyo wa masomo na kuhakikisha ufaulu wake unaongezeka na kufikia divisheni ya kwanza ya alama tatu.

Mwanafunzi Mariam akiwa pamoja na wafadhili TBC, Mwanza University na Benki ya NMB

Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Mhe. Gift Msuya akipanda mti kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa.

Hafla ya upandaji miti mji wa Serikali - Mtumba

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa, Juni Mosi, alishiriki kama mgeni rasmi katika zoezi la upandaji miti katika Mji wa Serikali Mtumba uliopo Mkoa wa Dodoma ikiwa ni katika kuelekea maadhimisho ya kilele cha siku ya mazingira Duniani ambayo huadhimishwa kila mwaka ifikapo June 5.

Lengo la kupanda Miti katika Mji huo wa Serikali ambao ndipo yanapojengwa majengo ya Wizara na Taasisi mbalimbali ni katika jitihada za kuufanya Mkoa wa Dodoma kuwa wa kijani kwa kupanda Miti zaidi ya Laki Tano kwenye Mji huu ili kukabiliana na Ukame ambao ni asili ya Mkoa wa Dodoma.

Mji wa Serikali Mtumba unahusisha ujenzi wa Majengo ya Taasisi za Kiserikali, miundombinu ya Barabara zenye urefu wa Km 51.2 ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 99 mpaka sasa na tayari ofisi 23 zimekamilika huku Serikali ikitoa Shilingi Bilioni 300 ili kukamilisha majengo yaliyobaki.

Ujenzi wa Mji wa Serikali, Mtumba, ulianza mwezi Novemba 2018 ukiwa umepangwa kuhusisha maeneo ya biashara, vituo vya magari ya abiria, hoteli za kitalii, huduma za kibenki, maofisi, jingo la Sinema pamoja na majengo makubwa (Shopping Malls). Pongezi nyingi zimetolewa kwa Rais Samia kwa kuwezesha fedha za ujenzi wa awamu ya pili wa majengo 24 ya ghorofa, Ofisi za Mabalozi na jengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kongamano la Mkoa wa Dodoma kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan

Mhe Mtaka akizungumza na Watumishi wa Dodoma

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma chini ya Mhe. Anthony Mtaka, iliandaa Kongamano la kumpongeza na kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan lililofanyika Mei 30, 2022 katika ukumbi wa PSSSF na kuhudhuriwa na Watumishi wa sekta mbalimbali za halmashauri ya Mkoa wa Dodoma.

Kongamano hilo lilitawaliwa na pongezi na shukrani nyingi kwa Rais Samia kwa uthubutu aliofikia wa kuongeza mishahara na posho za safari na kujikimu kwa Watumishi wa Umma ambapo watumishi kutoka kada mbalimbali waliopata nafasi ya kutoa shukrani zao, walisema kuwa ongezeko hilo litaongeza ari, morali na kasi ya kufanya kazi kwa bidii pia itaboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Viongozi wa Taasisi mbalimbali pia walitoa pongezi nyingi kwa Rais Samia kwa kuendeleza na kuanzisha miradi mingi ya kimaendeleo hasa kwa Mkoa wa Dodoma ambao ndio makao makuu ya nchi. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa barabara za mizunguko (Ring roads), Uwanja wa ndege wa kimataifa wa Msalato na miradi mingine mingi ikiwemo mchango alioutoa wa Bilioni 2 za kukamilisha ujenzi wa soko kubwa la wamachinga.

Hivyo hatua hizi zitasaidia kufungua uchumi wa mtu mmoja mmoja, Mkoa na Taifa kwa ujumla.

Watumishi wa Dodoma wakisikiliza mada mbalimbali

Upandaji miti Shule ya Msingi Mvumi Makulu

Katika kuelekea Kilele cha siku ya Mazingira Duniani, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma iliendelea na zoezi la upandaji miti kwenye maeneo mbalimbali ambapo siku ya Jumamosi June 4, 2022 zoezi hilo lilifanyika katika shule ya msingi na sekondari Mvumi Makole.

Zoezi hilo lililosimamiwa na Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Bi Gift Msuya, lilifanikisha upandaji wa Miti 3,000 katika eneo la Shule hizo huku wadau mbalimbali wa Mazingira wakishiriki kama vile Wakala wa Misitu (TFS), Lead Foundation (Kisiki Hai) na Chuo Kikuu Cha Dodoma (UDOM) ambao wamefaniisha upandaji na utunzaji wa Miti katika maeneo mengi ya Mkoa wa Dodoma tangu kuanza kwa kampeni ya kuifanya Dodoma ya Kijani.

Wanafunzi wa shule ya Msingi na Sekondari Mvumi Makulu wakisikiliza hotuba wakati wa halfa ya upandaji miti iliyoandaliwa na Ofisi ya Mkoa Dodoma

Mhe. Mtaka afanya mkutano wa hadhara na wakazi wa Kisasa

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Anthony Mtaka akisalimiana na baadhi ya Viongozi katika kata ya Kisasa

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Anthony Mtaka, alifanya Mkutano wa hadhara na wanachi wa Kisasa siku ya Jumapili Juni 05, 2022 lengo kuu likiwa ni kuzungumzia hali ya ulinzi na usalama wa eneo la Kisasa ambalo hivi karibuni yamejitokeza matukio mengi ya uvunjifu wa amani na kufanya wanachi kuishi kwa wasiwasi

Mkutano huo ulihudhuriwa na Kamati ya Ulinzi nausalama ya Mkoa na ile ya Wilaya, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Mkurugenzi wa Jiji, Kamanda wa Polisi wa Mkoa, Mbunge wa Jimbo la Dodoma, Meya wa Jiji na wananchi ambao ndio wahanga wa matukio ya kihalifu katika maeneo yao.

Changamoto mbalimbali zinazopelekea matukio ya uhalifu yanayofanywa na vijana wadogo wanaojiita "panya kaloa" ziliainishwa kama vile uwepo wa madereva wa Bodaboda wasio waaminifu, wanafunzi wanaotoroka shule au kuacha masomo pia uwepo wa maeneo yasiyoendelezwa ambayo ndio huzaa maficho ya wahalifu.

Suluhisho lililotolewa katika mkutano huo ilikua ni kuangalia namna ya ufungaji wa kamera za ulinzi (CCTV) kwenye maeneo ya biashara pamoja na kituo Mama cha bobaboda cha Kisasa sheli, ulinzi shirikishi, kuwany'ang'anya wale watakaobainika kushindwa kuendeleza maeneo yao kwa mujibu wa sheria na kuanza mara moja kwa ujenzi wa Kituo cha kudumu cha Polisi.

Sehemu ya wakazi wa kata ya Kisasa wakifuatilia mkutano kati yao na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Anthony Mtaka